

KAKAMEGA CENTRAL SUB COUNTY JOINT EVALUATION EXAM 2015

Kiswahili

Paper 1

Kiswahili insha 102/1

Mwongozo wa kusahihisha

1.Hii ni barua rasmi

-Sharti iwe na anwani mbili, ya mwandishi na ya mwandikiwa/mpokezi/mlengwa

-Tarehe iandikwe chini ya anwani ya mpokezi

-Mtajo uwekwe chini ya anwani ya mwandikiwa/mpokezi k.m.kwaBw/Bi.

-Lengo/sababu ya kuandika barua k.m.KUH./MINT.MATATIZO YANAYOWAKUMBA VIJANA
KATIKA ENEO LA NISHATI.

-Iwe na mwili inayo jadili matatizo hayo kwakina .Matatizo haya yapangwe kiaya.

-Iwe na hitimisho.

-Iwe na sahihi, jina na wadhfa wa mwandishi

Matatizo ya vijana yajumuishwe

-Ukosefu wa ajira

-Utumizi wa mihadarati

-Ukosefu wa usalama

-Mimba za mapema

-Ukosefu wa karo ya kujiendeleza kielimu

-Ukosefu wa pesa za kuanzisha miradi.

-Shinikizo la rika

-Utandawazi-matumizi mabaya yavyombo vya mawasiliano

-Pengo kuu la kizazi

-Uozowa jamii

Hoja nyingine za watahiniwa zikaridiwe ipasavyo

Kutuza:-Atakayekosa kuzingatia vipengele vyote vya barua atakuwa amepugukiwa kimtindo

-Atakaye andika insha nyingine tofauti na barua atozwe makinne.(4)

-Atakaye zungumzia mambo tofauti na matatizo atakuwa amejitungia swali,asituzwezaidiyakiwango
cha D-,maki 1- 2

-Atakayekosa kurejelea eneo la nishati atakuwa amepungukiwa maudhui.

2.Mtahiniwa ajadili/afafanue kwa kina njia mwafaka zinazoweza kutumiwa na serikali kupambana na tatizo
la gharama ya juu ya maisha nchini Kenya.arejeele yafuatayo

-Kupunguza bei ya bidhaa ya kimsingi

-Kupunguza/kufutilia mbali ada za huduma za kimsingi kama vile matibabu, elimu, n.k

-Kusisitiza ulipaji wa ushuru na wote

-Kupanua nafasi za kazi/ajira

-Kupambana na tatizo la ufisadi

-Kuhimiza wananchi na mashirika mbalimbali kubuni nafasi za kazi

-Kupunguza/kuunganisha idara mbali mbali za serikali kuu na kaunti

3.Hii ni insha yamethali. Mtahiniwa aelewe kuwa methali ina sehemu mbili na aishughulikie kikamilifu.

Maana ya nje ni kuwa ndege wengi hujenga viota vyao kwenye mti mkubwa na hivyo basi ukianguka,
ndege hao huteseka kwa kukosa makazi.

Maana ya ndani ni kuwa mtu mkuu anayetegemewa na wengi anapoondoka,wanaomtegemea huteseka kwa
kukosa mwelekezi.

Mtahiniwa atunge kisa au visa vinavyo afiki hali hii.

Arejeele wafuatao;

-Mzazi ambaye kuondoka kwake kulisababisha kusambaratika kwa familia yake

-Kiongozi yeyote ambaye kuondoka kwake kuli sababisha utengano, migogoro katika sehemu yake ya
uongozi n.k

Mtahiniwa aonyeshe waziwazi dhana ya mkuu kutegemewa na namna waliomtegemea walivyoathirika
baada ya kuondoka kwake.

Kutuza

-Si lazima aeleze maana ya methali

-atakaye rejelea maana ya nje pekee, atakuwa amepungukiwa maudhui. Asituzwe zaidi ya kiwango cha C maki 8

-Asiyezingatia sehemu mbili za methali kikamilifu, atakuwa amepungukiwa kimaudhui.

-Atakaye andika insha isiyo na uwiano wowote, atakuwa amepotoka , atuzwe D+ maki 3

4. Hii ni insha ya mdokezo mtahiniwa sharti aanze na maneno aliyopewa.

Kisa kilenge safari yoyote, jinsi ilivyoanza nakuisha.

Yaweze kuwa ilimalizika vizuri au vibaya.

Mtahiniwa ajihusishe na matukio ya safari husika.

Yaweza kuwa safari halisi , yakimawazo au ndoto.

Kutuza

-Mtahiniwa sharti aanze na maneno aliyopewa , asiyeanza kwa maneno haya lakini ayaweke katika insha yake atakuwa amepotoka, atuzwe kiwango cha D+ maki 3.

-Atakaye kosa kuyaweka maneno haya katika insha yake atakuwa amepotoka , atuzwe maki 1-2 kiwango cha D-

-Atakayekosa kushiriki katika safari husika atakuwa amepungukiwa kimaudhui akadiriwe ipasavyo.

KAUNTI NDOGO YA KAKAMEGA YA KATI

KISWAHILI 102/2 MWONGOZO

1. UFAHAMU

- a) Wanawake /nafasi ya wanawake katika jamii/ dhuluma kwa wanawake nk
(1x1 =1)
- b) i) Mafuriko
ii) Ukame
iii) Milipuko ya Volcano (3 x 1 =3)
- c) i) Umaskini / kuishi katika mazingira magumu
ii) Mapendeleo ya kisera na kitamadni yanayowadharau na kuwapuuza wanawake
iii) viongozi wa familia / kupambana na uongozi wa familia pamoja na uzalishaji / kuachiwa majukumu ya malezi / kutunza jamaa za mzazi mmoja bila usaidizi wowote
zozote (3x1=3)

d) Majukumu ya kijamii na kitaifa

- i) Wao ni chanzo cha ngucu kazi / wao na watoto wao hutekeleza kazi nyingi nyumbani na mashambani
ii) Wana uwexo bora wa kutunza chochote walichonacho
iii) Kuendelea kilimo ili kupata chakula / kusalisha chakula mashambani
iv) Kuandaa chakula nyumbani
Zozote (3x1= 3)

- e) i) Wanawake wa mataifa yaliyoendelea wameondolwea vikwazo mbeleyao iliwatekelexe wajibu wao. Ilihali way ale ambayo hayajastawi huchukuliwa kama watumwa/ watumishi vifaa/bidhaa
ii) Wanawake wa mataifa yaliyoendelea hudhaminiwa na wanauma kama wenzao katika ujenzi wa jamii ilhali wa mataifa yanayoendelea huwa chukulia watumwa/ watumishi vifaa/bidhaa
yoyote (1x2 =2)

f) i) Uchochole – umaskini / ufukara / ukata

- ii) Kudhalilisha – kudunisha / kudharau/ kukandamiza/ kutesa/kunyanyasa
iii) Mitafaruku- Migogoro/ mivutano/ mikinzano
(3x1=3)

Makosa

s- ondoa $\frac{1}{2}$ alama kosa linapotekea mara ya kwanza. Usizidi, , nusu ya alama alizopata katika kishemu
h- $\frac{1}{2} \times 6 = 3$

2. UFUPISHO


- a)
- i) Fikira inayotawala, sasa ni jela si mahli pa adhabubalimatibabu
ii) Wataalam wa urekebishaji tabia wamesema mhalifu akiadhibiwa sawa kifungoni huwa sugu zaidi
iii) Wanasisitiza lengo la kumtia mtu jela liwe kumjenga kitabia
iv) Wahalifu waspobadilishwa tabia gerezani huhatarisha zaidi maisha ya watu watokapo gerezani
v) Baadhi ya wahalifu wamefaidika kutokana na vifungo vyao

- vi) Magazeti na vyombo vya habari huvutiwa na maisha ya wafungwa
- vii) Sinema nyigi zimetungwa kufuata maisha ya wahalifu fulani
- viii) Watetezi wa haki za kibinadamu wanadi kuwa wanayotendewa wafungwa ni kinyume cha haki za kibinadamu
- ix) Magereza mengi yanakarabatiwa kuyapa ubinadamu
hoja zozote (6x1)

b)

- i) Wafungwa wanashughulikiwa kwa kila hali
- ii) Wafungwa wanapata chakula chenye viinilishe bora
- iii) Wafungwa wanapata malazi bora na maji safi
- iv) Wafungwa wanapata elimu, kuhudhuria madarasa na kutahiniwa kitaifa
- v) Wanaishi katika mazingira nadhifu
- vi) Kuna mashindano ya michezo na urembo kwa wafungwa wakike
- vii) Wafungwa wanasoma magazeti na kutazma runinga kupata habari
(zozote 7x1 = 7)

Kutuza



Makosa – Ondoa

$$s - \frac{1}{2} \times 6 = 3$$

$$h = \frac{1}{2} \times 6 = 3$$

Ziada – Maneno kumi ya ziada ya kwanza ondoa al 1.

Kila maneno tano – $\frac{1}{2}$

3. MATUMIZI YA LUGHA

- a) Mwalimu kijana ameajiriwa shuleni

V – nomino

Askari jela amemtesa mfungwa

V- nomino

(1x1=1)

- b) i) Vielezi hamna mfanano- Hutumia Ki- mfanano kuelezea kitendo kinacyotendeka, kwa kulinganisha
- Hufananisha vitendo na vivumishi/ nomino kwa kutumia “ki”

Vielezi namna hali- Hutufahamisha hali ambamo kitendo kilifanyika. Hujihusisha na tabia ya kitu/ mtendaji wa kitendo

(2 x 1=2)

- ii) Alicheza kitoto/ kiungwana / kinyama/ kiganda/ kivivu

- c) Chuuza –uza vitu kwa kuvitembeza

Chuzua – chagua kitu kwa sababu ya kuwa bora

$1 \times 2 = 2$ akitunga sentenzi mbili = 0

d) Naam – kihisishi (I)

Kabla ya – Kihusishi (H)

Yule – kivumishi Kiashiria

$(3 \times 1 = 3)$

e) Hapo napo ndipo nitakapo ($1 \times 1 = 1$)

f) Simba aliyepigwa risasi ameumizwa vibaya sana

(N + S) + (T + E + E)

KN 1

KT 1

$(2 \times 1 = 2)$

g) Matumizi ya kinyota *

Kuonyesha neon litaelezewa zaidi chini ya ukurasa / tambihi

i) Kuonyesha maendelezo yasiyofaa ya neon k.m mashairi

ii) Kuonyesha sentensi ina mpangilio mbaya wa maneno kw Baba kile chakula alikila

iii) Kuonyesha neon ni la lugha ya kigeni Km “matoke” irio

iv) Kutoa tahadhari km *hakuna njia hapa

h) Wa kijinsia – RH (Kinai kihusishi)

i) Kiongozi mwenye msimamo –RN (Kirahi nomino)

j) i) Vitendo vyote vitendwe kwa niaba y ake

ii) vitendo vyote vitendwe kwa sababu yake/ kwa ajili yake

(2×1)

k) Mwalimu alimwambia mwanafunzi Yule kuwa michezo yao ya mpriaingeng’oa nanga siku ambayo ingefuata

$(\frac{1}{2} \times 4 = 2)$

l) i) Fatuma, Khamisi mjukuu wa Rashid na Rehema wametoroka shule

ii) Fatuma, Khamisi, mjukuu wa Rashid na Rehema wametoroka shule

iii) Fatuma Khamisi, mjukuu wa Rashid na Rehema wametoroka shule

$(\text{zozote } 3 \times 1 = 3)$

m) i) po ya wakati

Po ya mahali $(2 \times \frac{1}{2})$

ii) Alipochelewa kufika shule aliadhibiwa

- Alipokuwa ameketi palikuwapachafu mahali

$(2 \times \frac{1}{2} = 1)$

h) Amri / Maagizo / maelekezo

$(1 \times 1 = 1)$

o) usibanduke papa hapa

Kiwakilishi kiwakilishi

Nafsi kiambato kiashiria kisisitizi

$(2 \times 1 = 2)$

p) Mpishi akiwa mwangalifu chakula kitaiva vizuri

$(2 \times 1 = 2)$

q) Mama alimunyweshwa mototo maziwa

$(1 \times 2 = 2)$

r)

S					
KN	KT				
N	T	H	N	V	E
Gofu	hushabikiwa	na	watu	wachache	sana

$$(1/2 \times 8 = 4)$$

MAKOSA

$$H = 1/2 \times 6 = 3$$

S = odoa 1/2 alama na sirudi 1/2 alama alizopat za kishemu

ISIMU JAMII

- a) i) kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya taifa na pia rasmi ilikutumiea katika shughuli zote rasmi km bngeni na ofisini.
ii) Kufunzwa shuleni kama somo la lazima na vyooini
iii) Katika vyombo vya habari hutumiwa katika matangazo na habari redioni, runinga na magazeti
iv) kuunda vyombo vya ukoraji na venezaji wa Kiswahili katika Nyanja mbali mbali km chama cha Kiswahili cha taifa (CHAKITA)
v) Hutumiwa kuendeleza shughuli za biashara
vi) Kutumiwa katika shughuli za kisiasa na utawala
vii) Kuruhusu uandishi, utafiti na uchapishaji wa vitabu katika lugha ya Kiswahili
viii) Kiswahili kuigizwa kwenye tarakilishi na mitandao ili kutumiwa katika mawasiliano (5x1) za kwanza tano
- b) i) Kuwepo na makabila mengi yenye lugha ambazo si za kibantu
ii) Wasemaji wengi wa lugha za mama wasiotaka kujifunza lugha ya Kiswahili
iii) Kuzuka kwa kijilugha cha sheng
iv) Watu wa tabaka la juu kupendelea kingereza kuliko Kiswahili
v) Kukosa walimu wa kutosha kufunza Kiswahili shuleni
vi) Wataalam wachache wa kukuza lugha
vii) Utafiti kamilifu haujafanyiwa taaluma ya Kiswahili kwa kukosa wafdhili
- (5 x 1)
Makosa
 $h = 1/2 \times 4 = 2$
 $s = 1/2 \times 4 = 2$

**KAUNTI NDOGO YA KAKAMEGA YA KATI
KISWAHILI 102/3**

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

1. (a) Ili asiwe na wasiwasi ya kutukanwa na huhiniwa aepuke kufanyiwa mabaya. $1 \times 2 = 2$

(b) (i) Pindu/mkufu/nyoka (al.1)

Kwa sababu neno la mwisho katika mshororo wa mwisho wa ubeti linatumiwa kuanzia ubeti unaofuata. (al. 1)

(ii) Ukaraguni (al.1)

Vina vya kati na vya mwisho vinatofautiana kutoka ubeti mmoja hadi mwingine. (al.1)

(c) (i) Tashbihi

- Hafifu kama muwele

- Tele mithili kitoto.(al.2)

(ii) Uradidi/Takriri

- Subira'

- Bora, kombora, ukora

- Kiburi, kudhuri n.k.(al.2)

(d) (i) Misuli kuwa dhaifu sana kama ya mgonjwa.

(ii) Hasa mgonjwa mwenye tatizo la

(iii) Ambao unasumbua sana daima na (iv) usiopona kwa vishale. (zote $4 \times 1 = 4$)

(e) (i) Inkisari - kuleta urari wa mizani k.m kilo — kilicho.

(ii) Tabdila - kuleta urari wa vina k.m. kudhuri — kudhuru maole — maozi.

- Kuleta urari wa mizani k.m nduwele — ndwele

muwili — mwili

(iii) Mazida - kuleta urari wa vina pia mizani.

- Vinitomele - vinitome.

Kutaja na matumizi (at.1)

Mfano (al.1)

Zote $3 \times 2 = 6$

KIDAGAA

2. (a) Imani iliajiriwa kazi kwa mwalimu majisifu. Alikuwa mtu wa kwanza kuwaona na kuwatendea utu watoto walemavu wa Majisifu (uk. 30) Majisifu aliwahirumia mkewe na Imani kwa ulezi wa watoto vilema. (uk. 137) Na kitambo aliwachukia na kuwaita masimbi na mashata. ($1 \times 2 = 2$)

(b) (i) Mtemi Nasaba Bora alimpenda msichana akiwa safarini na alipogundua alikuwa kiguru alimkataa (Uk. 100)

(ii) Dora aliwaficha watoto wake walemavu wageni walipoingia. (uk. 45)

(iii) Mashaka aliwachukia na kuwadharau watoto walemavu wa Amu yake. Aliwaona kuwa wasiokamilika au kama madubwasha.

(iv) Chwechwe Makweche alishabikiwa na watu wengi alipoitea sifa Songoa F.C. lakini alipovunjika fupaja hawakushughulikia hadi akakatwa mguu.

(v) Matuko Weye alifungiwa Sali na kupigwa (wazimu).

Zozote $3 \times 2 = 6$

(c) (i) Maakazi ya wakoloni yalij itenga nay a Wafrika.

(ii) Madhubuti baada ya kutoka Urusi alihamia kibanda cha Amani akajitenga na wazazi wake.

(iii) Ben Bella alipogundua lowela dadake ni rafikiye Mtemi Nasaba Bora alijitenga na Mashaka.

(iv) Uhasama wa mtemi ulifanya Majisifu nduguye kujitenga naye (Hakusherehekea na Mtemi kurudi kwa Madhubuti).

(v) Mtemi Nasaba Bora alimtaliki mkewe Zuhura kwa tuhuma za kuwa na uhusiano na Amani. (vi) Amani aliishi katika vibanda vilivyokuwa vimetengana na Kasri la Mtemi Nasaba Bora.

(vii) Mtemi nasaba Bora alitengana na Uhai kwa kujitia kitanzi kwa sababu ya shida zajimbo la Sokomoko.

(viii) Mwalimu Majisifu aliposhindwa kutoa mhadhara Wangwana katika chuo cha mkokoteni alijitenga na wanavyuoni na kurejea nyumbani.

(zozote $5 \times 2 = 10$)

3. Mvutano katikajamii ya Sokomoko.

(i) Mtemi na Madhubuti.

Madhubuti anakataa ufisadi, matendo maovu ya mtemi.

(ii) Mtemi na Amani.

Mtemi alishuku uhusiano kati ya Amani na Zuhura mkewa akamwadhibu vibaya. Amani alitaka kufahamu ukweli wa kifo cha babu Chichir. Hamadi na kufungwa kwa amu Yusuf Hamadi.

(iii) Mtemi na Zuhura.

Zuhura alikashifu ukatili wa Mtemi, kutowajibikia ndoa. Mtemi kumtaliki Zuhura kwa kumshuku kuwa mzinzi.

(iv) Dora na majisifti.

Dora hakufurahia ulevi na kutosaidiwa ulezi wa watoto walemavu. Majisifu anamlaumu Dora kwa kuzaa watoto walemavu.

(v) Mtemi na Lowela.

Lowela anamlaumu Mtemi kwa kuwafungia Imani na Amani kwa tuhuma ya kuu kitoto.

(vi) Majisifu na Mtemi.

Mtemi anakashifu aibu inayotokana na Majisifu kuwa mievi. Majisifu hafurahii ukatili wa mtemi k.m kumtesa Amani.

(vii) Mashaka na Ben bella.

Ben Bella anavunja uhusiano na Mashaka kwa sababu Mtemi Nasaba Bora alikuwa na uhusiano na dadake Lowela.

(viii) Imani, Amani na Wauguzi.

Wauguzi walikosa kuwajibikia kazi yao (mapuuza kitoto).

(ix) Mamake Imani na Askari.

Askari walimlazimisha ahame kutoka shambani licha ya kuwa na hati miliki.

(x) Majinuni na Michelle.

Tamaa ya michelle kutaka nyumba kubwa inapojengwa haimvutii (vyumba kumi na tatu). (xi) Amani na Majisifu.

Wizi na mswada wa Amani na kuchapishwa

(xii) Chwechwe makweche najamii.

Jamii kujivunia matokeo mazuri ya Songoa FC na kutomshughulikia alipovunjika fupaja. (xiii) Oscar Kambora na Mtemi.

Kunyakuliwa kwa shamba lao na askari kusababisha kifo cha mamake Imani na kuchomewa nyumba.

(xiv) Amani na wanafunzi chuoni Songoni. Walimwonea ghere kwa ufanifu wake masomoni kusababisha afungwe.

(xv) Matuko weye na Serikali (Uingereza na Sokomoko)

Baada ya kupigana katika vita vikuu vya dunia hakuzawadiwa alibaki kuwa kichaa.

(xvi) Mtemi aria mvutano nafsini mwake kuhusu maovu aliyoyatenda (uk 152). Zozote $10 \times 2 = 20$.

MSTAHIKI MEYA

4. (a) (i) Msemaji ni Meya

(ii) Msemewa ni Tatu (iii) Wako ofisini ma Meya.

(iv) tatu alikuwa ameinga wazo la wao kulipwa vizuri na kuonyesha tofauti ya usafiri kwa waajiri na watoto wao na wafanyakazi wengine.\

Zote $4 \times 1 = 4$ Meya

b. (i) Ni mwenye tama. Anaidhinisha nyongeza za mishara kwa madiwani iii yeye pia afaidike. (ii) Ni mwongo. Anadanganya kuwa wameagiza dawa kumbe hali sivyo.

(iii) Ni mwenye mapuuza. Anapoambiwa na Siki kuwa kitoto kimemfia Siki mkononi anasema huyo ni mmoja tu, Cheneo ma watu wengi.

(iv) Ni fisadi. Alinyakua viwanja vinane vya umma. Akampa Bili Vinnie.

(v) Ni katili anapoambiwa kuhusu kifo cha kitoto hajali asema huyo ni mmoja.

(vi) Ni mbadhirifu. Anatumia pesa za umma ovyo. Kuagiza mvinyo na divai, kutoka ng'ambo. Nyongeza za mishahara kiholela n.k

(vii) Ni mwenye majisifu. Anajisifia cheo chake na utajiri waka.

(viii) Ni mwizi. Alishirkiana na Bili. Diwani I, Diwani II kupanga njama ya kuiba na kuuza fimbo ya meya.

$$\text{Zozote } 5 \times 2 = 10$$

c. (i) Medi akana mgao si sawa na (ii) Beka kuongezea wakubwa hula kwanza na wao kupigania makombo.

(ii) Tatu anaongeza kuwa wanashindwa kulipia watoto wao karo na pia wanakosa kumudu gharama ya matibabu.

$$\text{Zote } 3 \times 2 = 6$$

5. VIONGOZI KUTOWAJIBIKA.

(i) Meya kukosa kustawisha mji wa Cheneo na kulinganisha ufanisi wake na miji midogo na dhaifu.

(ii) Meya kukataa kuonana na viongozi wa wafanyakazi. Na anapokutana nao anapuuza malalamishi yao.

(iii) Meya anapuuza mpango wa miaka kumi na kusema kuwa ana mipango ya millennia.

(iv) Mikutano ya baraza kufanywa kwa nadra, kama tunavyoelezwa na Diwani I kuwa inafanywa hasa wakati jambo kama mgomo kutokea.

(v) Meya anatoa ahadi za uongo. Alidanganya kuwa shehena ya dawa iko katika bahari kuu. (vi) Uchafu unaenea kila mahali na uvundo kukoleza hata ndani mwa majumba kwa sababu wafanyakazi wamegoma.

(vii) Meya anakataa kuongea na wanahabari kwa kisingizio kuwa ana wageni.

(viii) Badala ya kutunza fimbo ya Meya, wanakula kiapo kuficha sin za wizi wa fimbo.

(ix) Askari badala ya kutoa ulinzi wanawafursha watu kutoka mjini.

(x) Badala ya kustawisha Cheneo, anaagiza nyimbo za kizalendo zichezwe kabla na baada ya habari miaka hamsini baada ya uhuru.

(xi) Viongozi kujiongeza mishahara kiholela, kujilipa overtime na marupurupu ilhali baraza lina nakisi.

(xii) Meya kujifanya kuwa hajui watu wa Cheneo wanateseka (njaa, umaskini, magonjwa). Amefumbia macho matatizo yao.

(xiii) Meya kutoshughulika kuboresha elimu Cheneo na kuwapeleka wanawe ng'ambo kusomea huko.

(xiv) Diwani I na Diwani II wamekosa kuwajibika kama washauri wa meya wanampotosha badala ya kumkosoa.

(xv) Meya kutegemea ushauri wa mtu asiye na taaluma wala sifa za uongozi kwa mfano kesi ya mwanakandarasi, kuuza fimbo.

$$\text{Zozote } 10 \times 2 = 20$$

6. DAMU NYEUSI.

(a) (i) Ni maelezo ya mwandishi.

(ii) Akimrejelea Fikirini. Alikuwa Marekani kwa masomo.

Baada ya kuachwa na basi lililoendeshwa na mweupe (kubaguliwa) alianza kuona umuhimu wa nyumbani.

$$\text{Zote } 4 \times 1 = 4$$

(b) (i) Baada ya kuachwa na basi, alipotembea kando kando ya barabara kwenye kijia cha wapita njia akipepesuka kama mievi alikumbuka siku za hfahari alipotafuta Waragi Kibuye Kampala gongo Ubungo Tanzania na Changaa Mathare — Nairobi.

(ii) Alipotembea akipepesuka kwa baridi kali na theluji nyeupe aliona kila kiu cheupe na mweusi hana sauti na kudhalilishwa kwa mweusi na mweupe, alikumbuka maneno ya rais mstaafu moi, "msifikiri kwamba Mzungu anatupenda sisi watu weusi."

(iii) Alipokutana na kukaribiana na Fiona Mmarekani mweusi alikumbuka dada zake Wahaya aliokutana nao akiwa chuo cha walimu Mwanza, dada Waganda alipozuru Uganda Magharibi, dada Wakamba alipozuru Kitui..

(iv) Alipokuwa mkahawani alipewa chakula cha marekani ambacho hakukipenda alitamani chakula cha kwao ugali kwa mienda, wall na pilau, matoke na muhogo.

$$\text{Zozote } 3 \times 2 = 6$$

KIKASA

(b) (i) Kobe alitaka kupaa angani. Ni Bwana Mtajika alipotaka uongozi wa nehi ya tekede.

(ii) ndege walishirikiana na kobe kwa kumpa manyoya iii apate mbawa. Wanatekeda walishirikiana katika kumchagua Bwana mtajika kuwa kiongozi.

(iii) Kobe alipofika angani alijipajina Sisa wote akachukua chochote kilicholetwa kwa ajili ya wote.

Bw Mtajika alijaa ubinafsi akajilimbikizia mali na kuacha raia kwa njaa, umaskini na magonjwa.

(iv) Waliokuwa karibu na Kobe walibahatika kupata masalio (waliomfaa) Marafiki wachache wa Mtajika

kama Bw. Machupa ndio walinufaika kutokana na uongozi wake.

(v) Ndege waliamua kumnyonya Kobe manyoya yao na kumwacha arudi ardhini. Raia waliudhishwa na Bw. Mtajika kwa kutowajali na wakatumia kura zao kumwangusha.

(vi) Nani asiyeona gamba lake Bw Mtaj ika alipoondolewa mmlakani aliaibika na kushindwa kufurahia maisha.

Zozote $5 \times 2 = 10$

TAZAMANA NA MAUTI.

7. (a) (i) Lucy alitamani ajifanye mahututi na maradhi yake hayatibiki hapa pao. Lakini alifahamu kufika ubalozzi wa Uingereza ulijua ujanja huu na lazima daktari wao atoe ithibati kwanza.

(ii) Ajifanya anaenda kusoma. Ilibidi apate shule ambayo ingemkubali na awe na mtaji mkubwa wa fedha. Hakupita vizuri kidato cha sita na hakuwa na pesa.

(iii) Asema yeye ni mtalii tu, lakini angekuwaje mtalii na mifuko yake iwe mitupu? Hangekubaliwa Uingereza.

(iv) Rai ya kuolewa na mwanamume kutoka Uingereza. Kwa vile alikuwa na sura ya kuvutia lakini huyo mwanamme angetoka wapi? (Zozote $3 \times 2 = 6$.)

(b) (i) Kuwa na hamu kuu ya kupata kitu kasha matatizo yanakuandama.

(ii) Lucy alikuwa na tama kubwa ya kuwa tajiri haraka. Alitamani kwenda London iiii atomize ndoto yake.

(iii) Alitamani kupata mwanamme wa kumuoa iiii aweze kufika Uingereza.

(iv) Alikuwa na tama ya kupata raha huko London baada ya kurithishwa.

(v) Alitamani kuwa kama Yule niwanamke aliyekuwa katika Sinema.

(vi) Alidhani angekwenda London kama mkimbizi apewe pesa na ajifiche kutafuta pesa zaidi.

(vii) Aliolewa na (mzee na kwenda Uingereza na akamtunza lakini kabla ya kuhalalisha urithi wa mali ya Crusoe, Lucy kwa furaha alienda kujitembeza mjini na akapata ajali na kufa. (HOJA $7 \times 2 = 14$)

FASIHI SIMULIZI

8. (a) Majigambo au Vivugo. $1 \times 2 = 2$ (b) (i) Hutungwa na kughaniwa na mhusika mwenyewe.

(ii) Hutungwa kwa usanii mkubwa sana. Kwa mfano matumizi ya sitiari.

(iii) Anayejigamba hutunga kivugo kuguatia tukio mahususi katika maisha yake michezoni, vitani, kesi, jando na kadhalika.

(iv) Huwa na matumizi ya chuku. Mtunzi hujisifu kupita kiasi kwa kutaja mafanikio na mchango wake.

(v) Majigambo hutungwa papo hapo. Lakini mengine huandikwa na kughaniwa baadaye.

(vi) maudhui makuu ya maj igambo huwa ushuj aa.

(vii) Kwa kawaida hutungwa na kughaniwa na wanaume.

(viii) Anajigamba huweza kuvaa maleba yanayoana na kazi yake. Pia anaweza kubeba baadhi ya vifaa vya kazi.

(ix) Anayejigamba huweza kutaja na kusifu ukoo/nasaba yake.

(x) Mara nyingi wanaojigamba huwa Walumbi au washairi.

Za kwanza $5 \times 2 = 10$

(c) (i) Hukuza ubunifu. Mtunzi huirnarisha uwezo wake wa kubuni mitindo mipya ya utunzi na uwasilishaji anapoendelea kubuni majigambo.

(ii) Ni nyenzo ya burudani. Waliohudhuria sherehe huongolewa na majigambo.

(iii) Kukuza ufasaha wa lugha. Watunzi wengi wa majigambo huwa Walumbi ambao ni Weledi wa lugha.

(iv) Hudumisha utu na hutambulisha mwanamme katika jamii. Wanaume walipaswa kuwa Jasiri katika jamii kwa sababu ya uchokozi uliokuwepo.

(v) Ni nyezo ya kufanya watu waheshimiwe. Hufanya wanaume kuwa na an ya kuwa mashujaa.

Zozote $4 \times 2 = 8$